2. Kuwa na uwezo wa kuviwakilisha kijiografia vitu vilivyo kwenye mazingira.

Vifaa: Karatasi isiyo na mistari
'Wax crayons'
Penseli
Kionambali, chandarua za vipepeo, lensi ya kukuzia, chombo chenye vitu vya mazingira, compassi na vinasa sauti*
(*si lazima)

Njia:


1. Baada ya kuchagua eneo katika mazingira ya shule wanafunzi wataulizwa wanaelewa nini maana ya neno 'mazingira'. (Yaweza kufanyika kama utangulizi wa somo au mwisho ni, kuona kama wanafunzi wameielewa maana) dk 5.
2. Baada ya kueleweka kuwa ni "eneo linalotuzunguka" wanafunzi wataombwa kutafuta viumbe hai katika mazingira ya shule au alama ya vitu hai vilivyokuwepo. Ni muhimu kuangalia ufanikishaji wa zoezi hili pasipo kuharibu mazingira. dk 5.
3. Gawa vifaa vya kuchorea na onyesha nyenzo nyingine yoyote.
4. Wagawe wanafunzi katika makundi madogomadogo, wakati wa kuangalia alama, kama viota vya ndege, majani/magome ya miti, maua ndege, vipepeo, wadudu. Tafuta vitu vingi iwezekauavyo kwa dk 20.
5. Kusanyikeni tena kujadili vilivyopatikana. Toa maoni juu ya matokeo.

Nyongeza/upanuzi wa somo:

6. Darasani, chora ramaniya shule, na onyehsa wapi viumbe hai vimepatikana. Kwa wanafunzi wakubwa panua hadi kuonyesha kijiji, mito, na msitu wa hifadhi.
7. Sikiliza sauti, rekodi na tambua sauti.
8. Tumia vifaa vya kitaalamu zaidi katika kupima miti, kukusanya wadudu n.k.
9. Ingiza maneno ya kitaalamu zaidi katika uchunguzi wa Mazingira mfano, viumbe wasio na uti wa mgongo/wenye uti wa mgongo.
10. Badili msisitizo wa uchunguzi toka alama za vitu asilia kuangalia alama za matumizi/madhara yanayoletwa nabinadamu katika mazingira. Mifano ya madhara inaweza kujumuisha uchomaji moto, ulimaji, mabomba ya maji, matanuri ya matofali, ulishaji mifugo, matumizi ya miti kwa dawa. Hii inaweza kupelekea mjadala juu ya uwajibikaji katika mazingira mrudipo darasani.

Tathmini:

Itokane na mawazo ya wanafunzi na uelewa wa neno ‘mazingira’ na itokane na kazi za wanafunzi. Pia maoni ya walimu na yako binafsi.



Mwanafunzi akiandika vitu alivyoona katika Uchunguzi wake wa Mazingira

3. Kuhisi Kuna Nini Ndani ya Mfuko?

Mkazo: Sayansi/Lugha

Umri drs: 6+

Muda dk: 30

Shabaha: Kuongeza ufahamu wa kujua aina mbalimbali za viumbe hai waliomo ndani ya hifadhi ya msitu.

Malengo: 1. Kusaidia utambuzi wa viumbehai
2. Kuongeza matumizi ya lugha ya kujieleza.

Vifaa: Mifuko/makapu yenye vitu; mawili katika kundi la watu wapatao 10. Vitu/maliasili zilizopatikana msituni, manyoya ya ndege, matunda yenye mbegu ndani, mbegu, viota vya ndege, nywele, sufi, majani ya miwato n.k.

Njia:


1. Itaelezwa kuwa kuna vitu ndani ya mifuko/makapu kutoka msituni. Wanafunzi watakaa katika makundi yenye wastani wa watu 10 katika mduara na mfuko/kapu litapitishwa kuzunguka.
2. Pasipo kuchungulia, wanafunzi wataingiza mikono ndani ya kapu na watalinsi kilichopo. Watatakiwa kusema neno moja kuelezea kuna vitu gani, kila mara lazima liwe neno tofauti na la kwanza.
3. Kisha vitu vitafunuliwa polepole kuonyesha kama walikuwa sahihi.

Upanuzi/Nyongeza:

Sauti zinaweza kupigwa katika radio na kisha watoto/wanafunzi wakachora aina ya wanyama watakaoweza kusikia kwa. dk 5. Baadae sauti zitapigwa tena na kutoa maelezo kila sauti ikisikika (kwa kuandika/kuchora ubaoni ili kufafanua).

Tathmini:

Kukaza uwezo wa wanafunzi wa kubuni na kuongezeka kwa ujuzi.



Mfanyakazi wa kujitolea akionyesha ‘nini kimo kapuni’ kwa kundi la watoto.

4. Kitabu cha Kundi Kuandika Hadithi

“Siku Moja Nilikwenda Msituni na Niliona...”

- Mkazo:**
1. Ufahamu wa Mazingira
 2. Lugha
 - 3 Uchoraji

Madhumuni:

Kusisitiza umuhimu wa misitu katika maisha ya kila siku katika eneo husika, na Umuhimu wa wenyeji katika utunzaji wa mazingira. Kuonyesha uwiano wa maisha ya viumbe hai katika misitu.

Makusudi:

1. Kufikiria hadithi iliyotengenezwa vizuri yenye mwanzo, ukati na mwisho unaoeleweka.
2. Kwa kutumia misamiati na misemo inayotambulika.
3. Kujadili matatizo yanayoathiri misitu.
4. Kujadili jinsi ya kutunza misitu.

Vifaa:

Matangazo/mabango anayotumia Bwana miti yanaweza kutumika kama kikumbushio. Ubao na chaki, (ubao mweupe), kipande cha karatasi chenye matangazo.

Mbinu/Njia:


1. Watoto wataulizwa ni wanyama gani wanategemea kuwaona msituni, watu wanaweza kuutumia vipi msitu na nini kinaweza kuudhuru msitu. Mawazo yao yataandikwa/yataorodheshwa ubaoni.
2. Baadae itaelezwa kuwa wataandika hadithi ya pamoja. Mwalimu atanzisha hadithi kwa kuandika ubaoni “siku moja, nilikwenda msituni na niliona...” na kuuliza mtoto mmoja kuchangia mstari unaofuata, kwa mfano kwa kutumia mnyama. Mapendekezo jinsi ya kuelezea kilichoonekana yataombwa kuifanya hadithi iendelee.
3. Sentensi zitaandikwa ubaoni (na mwandishi ataandika hadithi jinsi inavyoundwa katika kitabu cha darasa). Kimantiki baada ya kuanza, kutakuwa na maelezo ya kujenga mandhari. Baadaye, jinsi hadithi inavyoendelea kuundwa shughuli za kati za hadithi zitamalizika (kwa uzuri au ubaya) mwishoni mwa hadithi.
4. Kwa watoto wakubwa (madarasa ya juu). Ukati wa hadithi utakuwa kama sentensi 10 na kumalizia kwa ‘ujumbe’.

Mwendelezo wa Somo:

5. Inawezekana mtindo huu kutumika na watoto wadogo pia. Hadithi ya mfano itasomwa darasani kuonyesha nini kinatakiwa.
6. Hadithi za mtu mmoja mmoja za watoto.
7. Kuelezea kitabu cha darasa.

Tathmini:

Shughuli hii yaweza kuwa kama zoezi la kukamilisha muunganiko wa kila kilichofundishwa wakati wa ziara. Shughuli hii (au shughuli ya Uchoraji wa Mabango) itumike kama somo la kuhitimisha shughuli. Tathmini inaweza kufanyika kutokana na uzuri wa hadithi, n.k.



Moja ya hadithi ya mwanafunzi mmoja mmoja

5. Kusanifu Tangazo (Bango)

Mkazo: 1. Ufahamu wa mazingira
2. Kuchora/kusanifu

Lengo: Kuonyesha ufahamu kuwa wote tunamiliki misitu na tunahitaji kufanya kazi pamoja ili kuhifadhi kwa ajili ya siku zijazo.

Umri drs: 5+

Muda dk: 30

Makusudi: 1. Kupanga kwa ufupi ujumbe juu ya jinsi ya kutunza msitu wa hifadhi.
2. Kuweza kuchora ujumbe kwa njia husika.

Zana:

Karatasi aina ya A4
Michoro mbalimbabli na kalamu za kuchorea.

Mbinu/Njia:


1. Katika kipindi cha Maswali na Majibu, wanafunzi wataulizwa kwa nini msitu ni muhimu na nini chaweza kudhuru msitu mfano uwindaji, uchafuzi wa maji, upasuaji mbao. Njia za kutunza msitu zitajadiliwa wakati huu. Maoni yataandikwa ubaoni.
2. Watoto watatakiwa kuchora/kusanifu bango la kushawishi watu kutunza msitu kwa matumizi ya baadae.

Mwedelezo wa Somo:

Kwa watoto wakubwa (miaka 8+) mawazo na vitu vya kuchora vinaweza kufanya vigumu zaidi, na bango linaweza kuwa na maelezo mengi zaidi.

Tathmini:

Shughuli hii inaweza kuwa kama zoezi la kukamilisha muunganiko wa kila kilichofundishwa wakati wa ziara. Shughuli hii (au shughuli ya Kitabu cha Darasa) itumike kama somo la kuhitimisha shughuli. Ni vizuri baadhi ya mabango yakatunzwa kama kielelezo au yakachukuliwa kutoka shuleni baadaye.



Bango la mazingira la mwanafunzi.

6. Meza ya Utambuzi

Mkazo: 1. Utapakao wa vitu asilia.

Umri: 5+

Urefu wa somo: dakika 30

Madhumuni: Kuhamasisha uelewa wa vitu asilia kwa kufanya mchezo wa kuamua kutambua vitu.

Lengo: 1. Kuongeza ufahamu wa watoto wa asili inayowazunguka.


Zana: vitu asilia toka msituni, mfano fuvu, gamba la nyoka, nyumba ya konokono, maotea ya mti, gome la mti.

Mbinu:

1. Panga vitu vyenye kutia hamasa kwenye meza na uliza watoto waeleze ni mnyama/mmea gani vitu hivi vimetokana navyo.

Mwendelezo wa somo:

2. Watoto wanaweza wakakusanya vitu vyao wenyewe na kutengeneza meza yao ya utambuzi. Wanaweza wakachora wanyama/mimea ambayo vitu vimetokana navyo na kufikiria tabia ya vitu hivyo.



Picha inayounganisha kipengele cha msitu na wanyama wake

3. ANDALIO LA KAZI

Author: Oliver, S.A. Pp. 73-111.

1. Chemshabongo

Madhumuni: 1. Kuongeza ufahamu wa bioanuwai katika msitu wa hifadhi na umuhimu wake.
2. Kukuza ujuzi wa lugha.

Lengo: Kuendeleza ujuzi wa kusoma na tahajia (spelling) na ung'amuzi wa maneno katika chemshabongo.

Vifaa: Karatasi ya chemshabongo
Penseli za kuandikia


Mbinu/Njia:

1. Mwalimu ataeleza chemshabongo ni nini (au atawauliza watoto wakubwa kuelezea maana), k.v. maneno yanaingiliana na majibu yamefichwa katika maelezo.
2. Soma maelezo ya kwanza kama mfano na jaza jibu. Kisha onyesha kuwa kila neno linalokatiza jingine ile herufi, pale yanapounganika, lazima iwe katika kila neno, na katika sehemu sahihi. Jaza jibu la pili kama kuna ulazima huo. Gawa karatasi za chemshabongo.

Tathmini: Matokeo ya kazi yenyewe

Mwedelezo wa somo:


Kwa namba na maneno magumu zaidi.

Mfano chemshabongo**CHEMSHABONGO 1****Kamilisha jedwali hili hapo chini****Kwenda kulia**

1. Mnyama mdogo hutoa sauti usiku.
2. Kinatumika kupikia chakula.
3. Unaweza kupata maji kutoka humo.
4. Anafanana na binadamu, huishi msituni.
5. Mti utumikao kupanda kwenye mpaka wa msitu.
6. Ndege anayeruka usiku na kupiga kelele ya 'uuuuuh'.

Kwenda chini



1. Mdudu arukaye, huliwa na ndege.
2. Kama nyoka, lakini ana miguu.
3. Aina ya mti wenye matunda makubwa yanayoliwa na yanautonvu.
4. Mahali palipoota miti na wanaishi wanyama pia.
5. Hutembea pole pole na nyumba yake mgongoni.
6. Mnyama huyu hupaa usiku na anapenda kuning'inia.
7. Mnyama mdogo mwenye shurubu na mkia.
8. Ndege mkubwa anayependa ku chukuwa wanyama.

CHEMSHABONGO 2Kamilisha jedwali hili hapo chiniKwenda kulia

- 2) Mnyama mdogo anapenda pombe.
- 4) Binadamu.
- 6) Ni tegemeo la watu kwa kujipatia chakula na mazao ya biashara.
- 8) Mnyama anatumika kubebea mizigo.
- 9) Hali ya kuwepo mimea/maotea.

Kwenda chini

- 1) Mnyama jamii ya mbwa anaishi porini.
- 2) Nini kinabakia mti ukikatwa.
- 3) Ni maji yanayotiririka bondeni kwa uelekeo maalumu.
- 5) Ni shughuli inayohusisha kuua wanyama.
- 7) Unamchanganyiko wa miti, majani na wanyama.
- 8) Ni mnyama apaaye angani hasa usiku na hupenda kuning'inia.

Majibu 1**Majibu 2**

2. Kuunganisha Doti Kuchora Picha

Madhumuni: Kusaidia kuona na kutambua mazingira ya msitu.
Kusaidia wanafunzi kujiamini katika hesabu na namba.

Lengo: Kurahisisha namba zinazofuatana

Vifaa: Katatasi yenye vidoti-doti ambavyo ukiviunganisha vinatoa picha fulani au umbo fulani.
Kalamu za kuandikia na kuchorea za rangi.

Njia/Mbinu:

1. Kwa watoto wadogo, mwalimu anaweza kumchagua mtoto mmoja kuhesabu 'moja' na kisha mtoto wa anayefuata kuhesabu 'mbili', na kuendelea, kuona mfuatano/mwelekeo kutoka namba moja hadi nyingine.
2. Ama vilevile, mwalimu anaweza kuelezea tu kuwa kinachotakiwa ni kuunganisha vidoti kwa mfuatano wa namba na kuuliza mmojawapo ameelewaje kabla ya kugawa karatasi. Picha zitakazotokea zitakuwa za vitu vya asili vinavyopatikana msituni.


Tathmini: Ni kuona picha halisi ama umbo halisi lililotaki wa limejitokeza.

Mwendelezo wa somo:


Ugumu wazoezi unaweza kurekibishwa kutokana na namba za doti na maudhui ya picha. Picha zaweza kupakwa rangi baada ya kukamilika.

Mfano picha za doti-kwa-doti


Picha 1:




Picha 2:




Picha 3:




Picha 4:




Majibu:


1. Ua



2. Chura



3. Panya



4. Ndege

3. Kutafuta Maneno Katika Jedwali

Madhumuni: 1. Kuongeza ufahamu wa bioanuwai katika msitu wa hifadhi.
2. Kukuza ujuzi wa tahajia (spelling skills).

Lengo: Kuweza kuhawilisha utambuzi wa neno toka chini ya karatasi, kulikumbuka na kulingamua neno hilo katika mraba fito.

Vifaa: Mraba fito (jedwali) la maneno.
Kalamu za kuandikia

Njia/Mbinu:

1. Waonyeshe watoto karatasi ya jedwali na elezea kuwa maneno chini ya karatasi yamefichwa ndani ya mraba fito. Uliza ni jinsi gani maneno yanaweza kupatikana. Tafuta herufi ya kuanzia. Elezea nini kitatokea ikiwa zaidi ya neno moja yataanza na herufi hiyo.
2. Toa mfano uliofanywa na tafuta neno jingine katika orodha. Gawa karatasi za mraba fito/jedwali.

Tathmini: Kiasi cha maneno yaliyopatikana.

Mwedelezo wa somo:

Maneno magumu zaidi katika jedwali kubwa zaidi.

Mfano jedwali la maneno

Jedwali la maneno 1

Kwa kutumia jedwali hili tafuta maneno yenye maana kwa kuyazungushia viboksi, mfano ‘popo’.

p	o	p	o	m	m
a	j	u	a	o	l
n	a	m	i	t	i
y	n	t	a	o	m
a	i	o	n	p	a

popo

moto

miti

jua

mlima

jani

panya

mto

Jedwali la maneno 2

Kwa kutumia jedwali hili tafuta maneno yenye
maana kwa kuyazungushia viboksi, mfano 'bonde'.

b	u	n	d	i	o	d	r	a	t	k	l	m	m	n	b
o	v	w	u	e	h	u	n	i	m	a	w	i	n	g	u
n	l	l	o	u	j	e	r	j	k	i	m	a	g	u	n
d	k	j	r	m	a	j	a	n	i	w	p	l	t	a	y
e	o	a	u	i	o	d	k	v	n	a	l	s	i	u	v
j	k	t	m	t	o	t	i	l	y	d	f	k	y	m	m
t	u	m	b	i	l	i	o	a	o	n	e	b	m	l	a
s	p	a	t	s	s	l	w	k	n	s	h	g	m	l	u
h	e	n	k	n	y	n	b	e	g	a	h	y	e	l	w
y	p	f	w	y	p	a	n	y	a	v	u	a	a	u	a
b	o	h	k	a	n	o	u	g	n	b	t	g	m	m	u
k	o	r	o	n	g	o	s	n	y	u	k	i	f	b	h
m	s	y	k	i	p	e	p	e	o	a	h	k	y	e	a
s	b	a	a	u	o	a	b	v	k	i	p	a	n	g	a
i	w	s	h	y	p	y	f	y	a	o	g	m	v	u	a
t	h	o	n	d	o	h	o	n	d	o	m	g	u	h	o
u	k	i	l	e	l	e	t	p	c	h	u	r	a	l	i

bonde	kilele	korongo	mlima	mbega	panya
bundi	kima	majani	mmea	ndege	popo
chura	kinyonga	mauwa	moto	njia	shamba
hondo hondo	kipanga	mawingu	msitu	nyani	tumbili
jabali	kipepeo	mbegu	mtu	nyoka	upepo
jua	komba	miti	mvua	nyuki	watu

Majibu 1

p	o	p	o	m	m
a	j	u	a	o	l
n	a	m	i	t	i
y	n	t	a	o	m
a	i	o	n	j	a

Majibu 2

b	u	n	d	i	o	d	r	a	t	k	l	m	m	n	b
o	v	w	u	e	h	u	n	i	m	a	w	i	n	g	u
n	l	l	o	u	j	e	r	j	k	i	m	a	g	u	n
d	k	j	r	m	a	j	a	n	i	w	p	l	t	a	y
e	o	a	u	i	o	d	k	v	n	a	l	s	i	u	v
j	k	t	m	t	o	t	i	l	y	d	f	k	y	m	m
t	u	m	b	i	l	i	o	a	o	n	e	b	m	l	a
s	p	a	t	s	s	l	w	k	n	s	h	g	m	l	u
h	e	n	k	n	y	n	b	e	g	a	h	y	e	l	w
y	p	f	w	y	p	a	n	y	a	v	u	a	a	u	a
b	o	h	k	a	n	o	u	g	n	b	t	g	m	m	u
k	o	r	o	n	g	o	s	n	y	u	k	i	f	b	h
m	s	y	k	i	p	e	p	e	o	a	h	k	y	e	a
s	b	a	a	u	o	a	b	v	k	i	p	a	n	g	a
i	w	s	h	y	p	y	f	y	a	o	g	m	v	u	a
t	h	o	n	d	o	h	o	n	d	o	m	g	u	h	o
u	k	i	l	e	l	e	t	p	c	h	u	r	a	l	i

4. Nyayo kwenye Njia za Wanyama

Madhumuni: Kuonyesha kuwa wanyama huacha vidokezo vingi vya kuwepo kwao. Kuhamasisha ujuzi wa utambuzi wa alama baadaye.

Lengo: Kuhamasisha uangaliaji wa alama za wanyama na tabia zinazohusiana nao.

Vifaa: Karatasi za alama (mabango ya alama/nyayo) zinazohusiana na picha za wanyama (jina liwe chini).

Njia/Mbinu:

Yafuatayo ni mapendekezo ya matumizi ya karatasi za alama:

1. Mchezo mdogo darasani, alama ya unyayo itawekwa juu na kuuliza ni (picha ipi ya) mnyama anaweza kutengeneza unyayo huo.
2. Kama msaada katika maelezo, mf. kwa kichwa “Nani hutengeneza alama hii?” na mapito ya mnyama vyaweza kutoa utambuzi sahihi wa mnyama.
3. Karatasi ya mapito ya wanyama yaweza kutumika kufanya uchunguzi wa mazingira shuleni.
4. Kama ikiwekwa katika karatasi A4 (au ubao) alama zaweza kutumika kwa zoezi rahisi la kuhusianisha alama na wanyama kwa watoto wadogo.
5. Yaweza kuwa msaada (ubao wa kuchupia) katika uandishi wa hadithi.

Nyayo za njia za wanyama

 1. Nyani	 2. Fungo
 3. Nguchiro	 4. Pelele
 5. Digi digi	 6. Kuchakuro

5. Wanyama na Makazi yao

Madhumuni: Kuongeza ufahamu wa wanyama na mahitaji yao.

Vifaa: Vipande vya karatasi vyenye picha za wanyama, ubao na chaki.








Njia/Mbinu:

1. Elezea neno ‘Makazi’. Jadili wapi tunaishi na nini tunakula.
2. Baadae waambie watoto kufikiria wanyama wanaohitaji msitu kwa makazi. Chukua kipande cha karatasi chenye picha ya mnyama na lionyeshe darasa. Waulize wanadhani mnyama huyo huwa macho wakati wa mchana au kama hutembea usiku.
3. Ugawe ubao katika sehemu mbili kukiwa na ‘jua’ upande mmoja na ‘mwezi’ upande mwingine. Kwa kila mnyama aliyejadiliwa mbandike kwenye upande wa ubao kwa kutumia ‘selotape’ kutegemea kama hutembea mchana (diurnal) au usiku (nocturnal).







Mwendelezo wa Somo:

4. Rudia zoezi sasa kwa kuweka kila mnyama kwenye makazi yake, mf. Makazi ya msituni, shambani, nk. kwa kuandika makazi haya ubaoni.
5. Fundisha juu ya ‘mtiririko wa chakula’ (food chains) kwa kuwauliza watoto nini mnyama anaweza kula na nini kinaweza kumla yeye. Panga picha za wanyama ubaoni katika mtindo wa ‘mtandao wa chakula’ (food web).

Picha za wanyama wa mchana (diurnal)

		
Nyani	Kipepeo (hoho)	Balale (halala)
		
Mwewe (kinpanga)	Nyoka	Chura (jula)
		
Mbega (mbegha)	Hondo hondo (hondo)	Mtu (mntu)
		
Kuchakuro (nkenda)	Nofi (ntaa)	Mjusi (ghondo)
		
Kima (ndue)	Kinyonga (uvi)	Kono kono (kozwe)

Picha za wanyama wa usiku (nocturnal)

		
Popo (nundu/lipo)	Panya (ngoshwe)	Melesi
		
Digi digi (paa)	Kanu (ukui)	Perere (npee)
		
Bundi	Panya (ngoshwe)	Komba (nkomba)
		
Nguruwe (nguwe) (neni za Kisambaa)	Fungo	Nungunungu

6. Jaribio La Mazingira

SEHEMU YA KWANZA:

**Chagua jibu sahihi na ulizungushie duara.
Kuna majibu mawili si sahihi lakini moja ni sahihi.**

- 1. Kwa nini hatutakiwi kufua nguo mtoni pasipo kutumia ndoo au dishi?**
 - a) Kwa sababu tunapenda nguo zetu chafu.
 - b) Kwa sababu sabuni tunayo tumia inaweza kuchafua maji.
 - c) Kwa sababu hatutaki mikono yetu ipate maji.
- 2. Nini hutokea wakati chupa ya mpira au mifuko ya mpira endapo itatupwa ardhini?**
 - a) Inageuka kuwa udongo.
 - b) Inasaidia mimea kukua.
 - c) Haiozi.
- 3. Ni njia gani nzuri tungetumia kutupa mabaki ya chakula?**
 - a) Kufukia ilikuya fanya ya oze.
 - b) Kuzichoma ilikufanya moto mkubwa.
 - c) Kuzitupa uwanjani kuzunguka nyumba.
- 4. Tutapataje nguzo za kujengea pasipo kutumia njia haramu za uharibifu wa misitu yetu ya hifadhi?**
 - a) Kwa kununua nguzo mbali kutoka misitu mingine ya hifadhi.
 - b) Kupanda miti ya vitalu katika kijiji chetu.
 - c) Kwa kuchukua nguzo tu katikati ya misitu wa hifadhi.
- 5. Ni jinsi gani misitu ya hifadhi hurekebisha hali ya hewa.**
 - a) Kutowekupo kwa miti jua halitaweza kuwaka.
 - b) Miti huzuia theluji kutelemka.
 - c) Miti kufanya kukusanyika kwa mawingu kiasi kwamba mvua inaweza kunyesha.
- 6. Ni madhara gani yatokanayo na betri zilizokwisha kutumika ziwapo ardhini?**
 - a) Wanyama hutumia kuzimeza.
 - b) Hufanya mimea kukua haraka kuliko kawaida.
 - c) Zinavujisha sumu hatari ardhini.
- 7. Kwanini ni muhimu kuwa waangalifu na moto katika mashamba yetu?**
 - a) Unaweza kuunguza pasipo udhibiti.
 - b) Kwa sababu unafurahia kuangalia.
 - c) Kwa sababu tunawasha mara moja kwa mwaka.

SEHEMU YA PILI:

Jibu gani kati ya haya yafuatayo si sahihi?

Kati ya majibu yafuatayo, Manne ni sahihi na moja tu si sahihi.

Zungushia duara kwa jibu ambalo si sahihi, Jibu (a, b, c, d, au e) .Tumia penseli.

8. Misitu ya hifadhi ni muhimu kwa sababu

- a) Ndio vyanzo vya maji ambayo tunahitaji kwa maisha ya kila siku.
- b) Ni nyumba / makazi ya viumbe kama wanyama na mimea ambavyo ni ya kipekee ambavyo huwezi ukavipata sehemu nyingine yeyote hapa duniani.
- c) Inapatikana mimea adimu ambayo mara nyingine hutumika kwa madawa na mila za asili.
- d) Hutusaidia katika ukusanyaji wa kuni kwa ajili ya kupika.
- e) Tunaweza kutumia miti kwa vinyago, ujenzi na kuwindia wanyama.

9. Kwanini tunaweza makazi yetu na vijiji safi na mbali na uchafu?

- a) Husaidia kuzuia usambazaji wa magonjwa.
- b) Huweka vijiji vyetu bora katika mpira wa miguu.
- c) Kupunguza namba ya panya na viumbe waharibifu karibu na makazi yetu.
- d) Hufanya tujisikie na uwekaji wa vijiji vyetu vema.
- e) Kuongeza ubora wa udongo na mitaa yetu.

10. Kwanini ni muhimu kwa sisi kulinda mifumo yetu ya maji?

- a) Ili tuwe na maji ya kutosha ya kunywa kwa miaka yote.
- b) Ili tuweze kunywesha mifugo.
- c) Ili vijiji vingine visiwe na chochote.
- d) Ili tuwe na maji safi ambayo hutuweka salama kiafya.
- e) Kwa ajili ya kumwagilia mazao yetu kipindi cha ukame.

SEHEMU YA TATU

Maswali machache unayoweza kuongelea shuleni...

●Waweza vipi kukifanya kijiji chako kisiwe kimetapakaa uchafu?

Pengine waweza kuweka vifaa vya kukusanyia uchafu kwenye shule au sehemu nyingine za umma. Tumia mifuko iliyotengenezwa kwa nyuzi za asili n.k.

●Wapi yafaa kuweka uchafu wa vitu visivyotengenezeka upya (non-recyclable) kama vitu vya plastiki na betri za zamani?

Katika shimo lililotengwa na kijiji mbali na vyanzo vya maji na mashamba.

●Wajua jinsi ya kuotesha mti?

Inahitaji udongo mzuri na maji mengi kwa kuanzia.

●Tunawezaje kuboresha ufuaji wetu wa nguo?

Tunaweza kuchota maji mtoni katika ndoo na kumwaga maji ya sabuni mbali na mto ili yasichafue maji yetu ya kunywa (au ya vijiji vingine chini zaidi ya mto)

MAJIBU

1 b, 2 c, 3 a, 4 b, 5 c, 6 c, 7 a, 8 e, 9 b, 10 c.

7. Mchezo wa ‘Maji Safi’


Umri: 12+

Madhumuni: Kwa watoto kufikiri juu ya mambo yanayoharibu ubora wa maji nakukazia maarifa umuhimu wa kuweka vyanzo vya maji safi.

Zana: Ubao wa mchezo
‘die’ moja
Vihasabio (mf. vizibo vya soda).

Mbinu:


1. Kwanza jadilianeni mahitaji ya maji safi. Waulize watoto tunatumia maji kwa kazi gani (mf. kwa kunywa, kupikia, kuoshea na pia kwa mifugo yetu na mazao)
2. Waonyeshe ubao. Lengo la mchezo ni watoto wajifunze juu ya mambo yanayoharibu ubora wa maji na vilevile njia zinazoweza kuzuia uharibifu huu. Mtoto atakutana na haya matatizo jinsi anavyoutambaa ubao kwenda chini. Sehemu ya ANZA inawakilisha mwanzoni mwa chanzo cha maji, na sehemu ya MALIZA ni sehemu ya chini ya mto ambapo maji huchukuliwa kwa matumizi kijijini.
3. Wachezaji wawili au watatu wataweka vihasabio vyao katika sehemu ya ANZA
4. Mchezaji wa kwanza atazungusha ‘die’ yake nakusogeza kihesabio chake mbele miraba kadhaa kwa kiasi itakavyoonyeshwa na ‘die’. Kama mchezaji ataishia kwenye mraba ulio tupu, atatulia hapo hadi zamu yake tena itakapofika. Kama akifikia mraba wenye maandishi atasoma na kusogeza tena mbele au nyuma kutegemea na nini kimeandikwa.
5. Kila mchezaji atazungusha ‘die’ kwa zamu. Mchezaji atakayefika au kuvuka



MALIZA mwanzo ndiye mshindi.

Chora umbo kama hili juu ya karatasi ngumu na kata kwa pembeni yake. Kunja kipande ulichokata kiwe mfano wa boksi dogo (mfano wa ‘die’ hapo juu). Tia gundi sehemu ya pembeni (iliyotiwa kivuli) ili kufanya boksi liwe imara. Hii sasa ni ‘die’ yako!

Ubao wa Mchezo ‘Maji Safi’



8. Andaa Siku ya Mazingira

Madhumuni: Kwa shule kuwa na jukumu hai la Kukuza mwamko wa mazingira kwa jamii.

Zana: Karatasi za mabango
Kalamu za kuchorea, n.k.,

Mbinu:

Iweje Siku ya Mazingira:

1. Chagua siku katika kalenda (pengine inayoendana na Wiki ya Mazingira Duniani)
2. Kuwe na kipindi cha majadiliano kupata nini cha kufanya siku hiyo. Baadhi ya mawazo ya naweza kuwa:
 - Kutunga na kuimba wimbo wa mazingira.
 - Imba/ghani shairi la mazingira
 - Tengeneza mchezo wa kuigiza unaohusu masuala ya mazingira
 - Endesha shindano la mabango/uandishi wa hadithi
 - Alika mgeni (guest speaker)
 - Upandaji miti



Mfano wa bango lililotumika kutangaza Siku ya Mazingira

9. Karatasi za Maelezo Halisi ya Viumbe

Madhumuni: Kuongeza ujuzi wa bioanuwai za msitu wa hifadhi.

Lengo: Kukuza stadi za kusoma: ufasaha, umakini, lafudhi, ‘kusoma kwa maana’, kuweza kuelewa makala na kujibu maswali yanayoihusu.

Vifaa: Karatasi za maelezo halisi.
Karatasi zisizoandikwa.
Penseli za kuandikia na kuchorea.

Mbinu/Njia:

Yafuatayo ni mapendekezo ya matumizi ya karatasi za maelezo halisi.


1. Kusoma kwa makundi baadhi ya karatasi kabla ya kuuliza maswali.
2. Karatasi za maelezo zaweza kutumika kama ‘mbao za kuchupia’ kwa watoto kuweza kuandika maelezo yao ya uhakika kuhusu wanyama wengine.
3. Watoto waweza kutunga vitendawili vinavyohusu wanyama wakimalizia na swali “Je, mimi ni nani?”. (Pengine na picha ya mnyama ikiwa imefichwa kwa chini).

Mwedelezo wa somo:

Kwa ugumu na upana zaidi.

Maelezo

MAELEZO YA KWANZA **Misitu ya hifadhi**



Ni ipi?

Msitu wa hifadhi Mlinga ni moja kati ya hifadhi za milima ya Usambara Mashariki. Milima ya hifadhi imeanzishwa ili kutunza vyanzo vya maji na miti pamoja na viumbe adimu wa mimea na wanyama wanaoishi ndani ya misitu.

Unajua je msitu wa hifadhi ulipo?

Msitu wa hifadhi una mpaka uliosafishwa majani yote. Maboya ya simenti yanaonyesha kona zote za mpaka wa msitu wa hifadhi. Mistari miwili ya miti imepandwa.

Mtunzaji wa misitu ni nani?

Bwana miti ana wajibu wa kusimamia utunzaji wa misitu. Anazuia uchomaji moto, ukataji miti hovyoyote, na uwindaji wanyama adimu. Pia husimama utunzaji wa mipaka ya misitu.


Wanaelimisha wananchi kutumia mazao ya misitu kwa njia endelevu. Ni wajibu wetu sote kusaidia kutunza misitu yetu. Ni kwa mamufaa ya kila mmoja wetu na tunahitaji tuwe nayo karibu.

Misitu mingine ya hifadhi Usambara Mashariki.

Ipo misitu mingi ya hifadhi katika milima ya Usambara Mashariki na hifadhi asili-moja. Hifadhi nyingine ni pamoja na hifadhi ya mazingira asili Amani, hifadhi ya Manga pamoja na hifadhi ya Segoma.

MAELEZO YA PILI

Moto



Ni nini?

Moto ni kitu ambacho kila mmoja wetu anatumia kupikia chakula. Utumikapo unafanya kila kitu kuwa cha moto. Mara nyingi tunatumia moto kutayarisha mashamba yetu. Tunaposhindwa kuudhibiti moto inakuwa ni hatari sana.

Ni nini moto wa msituni?

Moto huu hutokea pale eneo linapokauka sana. Mara nyingi watu huanzisha moto kwa bahati mbaya na husambaa schemu kubwa. Kwa sababu tunalima karibu na msitu. Moto wa mashambani pia huenea hadi msituni kwa bahati mbaya.

Kwa nini ni jambo baya?


Ni jambo baya kuchoma moto msitu kwa vile huteketeza wanyama na mimea muhimu ipatikanayo humo. Pia huunguza miti ya zamani ambayo ingetumika kama kuni za kupikia.

Nini cha kufanya tuonapo moto msituni

Tuonapo moto msituni ni vyema kutoa taarifa haraka kwa afisa misitu ili asaidiane na wananchi kupanga namna ya kukabiliana na moto huo. Tunatakiwa tujivunie na misitu yetu na tuhakikishe ipo salama.

MAELEZO YA TATU

Mimea maalumu



Misitu yetu ina aina nyingi za mimea isiyo ya kawaida na isiyopatikana sehemu nyingine duniani. Kuna aina ya mimea uitwayo "Dughulishi" (African Violet) upatikanao Usambara mashariki tu. Hutoa maua mazuri yenye rangi ya zambarau.

Nchi nyingine watu huotesha maua haya kwenye vyungu ndani ya nyumba zao kwa vile wanayaona ni mazuri.


Baadhi ya mimea ya msituni ina faida nyingi kwetu. Tunaitumia kwa madawa na kukipa chakula ladha. Kama tusingekuwa na misitu mimea hii isingeweza kuota.

Jaribu kufikiria miti yenye faida

Jaribu kuandika orodha ya mimea yote ambayo inatunufaisha.

MAELEZO YA NNE

Maji



Maji ni nini?

Maji huanguka kama mvua kipindi cha msimu wa mvua. Hujaa kwenye mito na hutusaidia kuotesha mazao yetu. Tunahitaji maji wakati wote kwa ajili ya kunywa sisi na wanyama wetu vile vile kwa ajili ya kusafisha vitu mbali mbali.

Tunatunza maji


Maji ni Uhai. Ni lazima tuhakikishe tuna maji safi na salama ya kutumia vinginevyo tutapata maradhi. Maji yatakuwa masafi endapo hatutayafulia ama kuyachafua. Wakati mwingine hapa Tanzania hatupati mvua ya kutosha hivyo ni vizuri kutunza njia zetu zinazo tupatia maji. Kwa kutunza miti na misitu yetu, mvua zitaendelea kunyesha mara kwa mara.

Miti inahifadhi maji kwenye majani, shina na mizizi. Bila miti ardhi itakuwa kavu. Miti inadhibiti kiwango cha maji ya mvua kwenye mito.

Angalia nje, mawingu yalivyosheheni maji na kujituliza kwenye msitu wakati wa mvua!

MAELEZO YA TANO

Miti



Miti ni nini?

Miti ni aina ya mimea mikubwa ipatikanayo msituni. Watu pia hupanda miti nje ya misitu.

Kwa nini tunahitaji miti?

Tunapata matunda na mbao za kujengea myumba kutokana na miti tunayopanda.


Tunaweza kuokota kuni kutoka kwenye misitu ya hifadhi lakini haturuhusiwi kukata miti iliyohai kwa sababu inashikamanisha udongo. Pia miti inatupatia hewa tuivutayo na kurekebisha hali ya hewa.

Ni nini kitatokea endapo hakutakuwa na miti?

Kama hakutakuwa na miti, hakutakuwa na mvua, maji ya kunywa na hewa tunayovuta. Pia hapatakuwa na mazingira ya kuota mimea pamoja na wanyama watakaishi msituni.

MAELEZO YA SITA

Nyoka



Nyoka ni nini?

Nyoka ni aina ya viumbe vyenye damu baridi vinavyoishi karibu duniani pote. Katika Afrika nyoka wengi wanaishi msituni. Watu wengine hawapendi nyoka kwa sababu wengine ni hatari na wana sumu. Ingawa wengine hawadhuru.

Nini unatakiwa kufanya umuonapo nyoka?


Kama utaona nyoka msituni tafadhali muache aende. Hawezi kukudhuru kama hukumkasirisha. Kitu muhimu cha kufanya ni kutomkaribia nyoka umuonapo.

Nyoka wa pekee

Milima ya Usambara mashariki ina aina ya nyoka wa pekee ambao hawapatikani sehemu nyingine duniani. Sehemu nyingine hufuga nyoka kama mapambo.

MAELEZO YA SABA

Nyani wa manjano



Nina ukubwa gani?

Ukubwa wangu ni kati ya (65-98sm) kutoka kichwani mpaka mwanzo wa mkiani. Nyani wa kiume huwa ni wakubwa zaidi ya majike.

Ninaishi wapi?

Nchi yote ya Tanzania zaidi katika ya misitu miombo lakini pia katika nchi kavu yenye vichaka na ukanda wa pwani. Ninahitaji majabali au miti kwa ajili ya kuishi kama nyumba. Ninahitaji kuishi karibu na maji ili kunywa maji kila siku. Nyani wanapatikana katika Bara la Afrika tu.

Ninakula nini?

Mbegu, majani na matunda. Pia maua, matunguu, maganda, magome, mizizina mashina. Chakula changu kikuu ni mboga mboga, lakini pia ninakula wadudu, nyoka na wanyama wadogo wadogo, vyura, kaa na samaki pindi wanapatikana.


Je, nina mlilo gani wa sauti?

Ukweli zaidi

Ninaishi katika makundi yenye nyani weginge wengi. Wanawake hutunza watoto wakati wanaume wanaangalia kila mahali. Kama walinzi wa kundi.

MAELEZO YA NANE

Mbega



Mimi ni nani?

Mimi ni mbega, jamii ya nyani.

Nina ukubwa gani?

Ukubwa wa kawaida kati ya (60-75sm). Mdogo kuliko nyani.

Ninaishi wapi?

Ninaishi katika safu pana ya mazingira kama - mianzi, misitu ya tambarare au nyanda za juu na milima, miombo na misitu ya vichaka vikavu.

Ninakula nini?

Zaidi majani, matunda na mbegu, lakini pia magome, nazi, na wadudu.


Nina mlilo gani wa sauti?

Ukweli zaidi

Ninaishi katika makundi, tunakaa katika misitu au miombo na hatuwezi kukatisha enco la wazi bila kusita. Kwa maana hii 'sisi tunatokana na misitu' au 'sisi tunategemea misitu' na hivyo tunahitaji misitu ili kuweza kuendelea kuishi.

MAELEZO YA TISA

Panya wa Afrika



Mimi ni nani?

Mimi ni Panya wa Afrika

Nina ukubwa gani?

Mimi ni mdogo sana. Ukubwa wangu ni sentimita 10 kutoka kichwani hadi mkiani. Urefu wa mkia wangu ni sentimita 13.

Ninaishi wapi?

Ninaishi msituni. Ninatengeneza kiota changu kwa majani makavu kwenge mashimo ya miti.

Ninakula nini?

Ninakula mbegu, majanina maotea wakati mwingine wadudu pia. Ninakula matunda yapatikanago msituni.

Ninakuwa macho wakati gani?

Ninakuwa macho usiku tu na nina lala mchana.


Nina mlio wa sauti gani?

Ukweli zaidi

Ninazaa watoto kati ya 1-5 wasio na manyoya, rangi ya hudhurungi na wasioona. Watoto kukuwa haraka sana na kuachana na mama yao majuma manne baada ya kuzaliwa.

MAELEZO YA KUMI

Popo



Mimi ni nani?

Mimi ni popo

Ninaishi wapi?

Ninaishi katika maeneo ya misitu na miombo katika Afrika yote isipokuwa Jangwa la Sahara. Ninaishi katika matundu ya miti, mapango na majengo.

Je, ninakula nini?

Ninakula wadudu, kumbikumbi na mchwa

Je, naweza kuonekawa wakati gani?

Ninaweza kuonekana nikiruka angani nyakati za usiku tu, hasa machweo na alfajiri (mawio).


Je, nina mlilo gani wa sauti?

Ukweli zaidi

Ninatoa sauti hizi kupitia pua yangu kubwa na siyo mdomo. Sauti hizi zina nisaidia nisigonge vitu kwenye giza. Mimi siyo ndege, ni mnyama kama wanyama wengine (kama vile Panya)

MAELEZO YA KUMI NA MOJA

Chura wa miti ya Usambara



Mimi ni nani?

Mimi ni chura wa miti ya Usambara. Kuna aina nyingi tofauti za vyura wa miti. Baadhi yetu tunapatikana tu katika safu ya milima ya ukanda wa mashariki ya Tanzania. Hii inatufanya tuwe wa maaana zaidi.

Ninaishi wapi?

Kama jina langu lisemavyo, ninaishi katika miti. Ninategemea misitu kuendelea kuishi. Pia ninahitaji maji kuweza kuishi na kutaga mayai.

Je, ninaonekana je?

Mimi ni chura mkubwa (sm 8.5) na mimi nina rangi ya kijani kibichi na bluu.

Na ninapatikana Usambara mashariki na mdogo zaidi.

Je, nima sauti ya namna gani?

Kwanini msitu wako ni muhimu kwetu?

Kwanza tunapatikana tu katika misitu ya ukanda wa milima ya mashariki. Tungekufa endapo msitu ungeharibiwa.

MAELEZO YA KUMI NA MBILI

Bundi wa Usambara



Mimi ni nani?

Mimi ni bundi wa Usambara.

Ninaishi wapi?

Kama jina langu linavyosema, mimi ninapatikana tu katika milima ya Usambara. Hii ina maana kwamba ninategemea misitu hii kuendelea kuishi.

Je, nina amka wakati gani?

Ninaa mka usiku ili kuwinda. Huwezi kuniona wakati wa mchana kwa sababu nitakuwa nimelala juu ya mti.

Je, ninafananaje?

Mimi ni ndege mzuri mwenye rangi nyekundu/hudhurungi kwenye mbawa na tumbo la rangi ya maziwa


Nina sauti gani?

Kwa nini misitu ni muhimu kwangu?

Kwa sababu mimi ninapatikana katika Usambara pekee, ninategemea misitu hii kuishi. Kama misitu ungeharibiwa nisingekuwa na mahali pa - kuishi.

MAELEZO YA KUMI NA TATU

Kinyonga



Mimi ni nani?

Mimi ni kinyonga shingo bapa(Flap-necked).

Ninapatikana wapi?

Ninaishi katika misitu ya mashariki na kusini mwa Afrika ikijumisha milima ya Usambara.

Je, ninakula nini?

Nina penda aina nyingi tofauti za wadudu kama vile panzi,inzi,buibui na vipepeo

Ninaonekana je?


Nina rangi ya kijani kinachong'aa na hukua mpaka urefu wa sentimeta 38. Nina sehemu kubwa (flap) inayojitokeza nyuma ya shingo yangu ambayo ninaweza kuitanua kama tembo anavyo piga piga masikio yake. Hili ni onyo kwa wanyama ambao wanaweza kutaka kunila mimi

Ukweli zaidi

Naweza kuzungusha macho yangu sehemu zote. Hii inanisaidia mimi kuona hatari na wawindaji (wanyama) kwa haraka (kama nyoka). Si sawa na baadhi ya vinyonga wengine, ninataga mayai. Wakati nikiangua mkia wangu unakuwa mrefu kama mwili wangu.

MAELEZO YA KUMI NA NNE

Pelele wa mtini



Mimi ni nani?

Mimi ni pelele wa miti. Mimi ni mnyama mdogo mwenye ngozi nyororo na sina mkia.

Nina ukubwa gani?

Mimi ni saizi ya kati, kati ya sentimita 30 hadi 60 kwa urefu.

Nina ishi wapi?

Ninaishi katika msitu na maeneo ya miombo hapa Tanzania. Nina tumia muda wangu hasa juu ya miti na wakati mwingine ninalala huko.

Nina amka wakati gani?

Mimi ni makini wakati wa usiku na mchana sioni.

Nina kula nini?

Ninakula majani, matunda, na matawi machanga juu ya miti. Wakati mwingine ninakula majani na mimea ardhini.


Ninatoa sauti gani?

Kwanini msitu ni mhimu kwangu?

Pelele wa mtini anapatikana tu katika milima ya Usambara, Upare, na Uluguru. Tunategemea misitu kuishi.

MAELEZO YA KUMI NA TANO

Popo wa matunda



Mimi ni nani?

Mimi ni popo wa matunda. Nina macho makubwa ya ugoro, na masikio yenye umbo la jagi.

Nina ishi wapi?

Ninapatikana Afrika nzima na pia bara la Asia na Australia. Nina ishi kwenye kundi kubwa na tunalala pamoja kwenye mapango au mitini.

Ninaamka wakati gani?

Nina amka wakati wa saa za usiku. Ninaweza kuonekana nikipaa au nikila kabla ya giza nene.

Ninakula nini?

Nina kula matunda, nta na maua ya miti.

Ninatoa sauti gani?

Ukweli mwingine

Kuna aina nyingi ya popo wa matunda wanaoishi katika sehemu hii ya Tanzania. Tunategemea msitu kuninginia na kula.